HOTUBA YA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA DR JAKAYA MRISHO KIKWETE KATIKA UZINDUZI WA MPANGO MKAKATI WA TATU WA SEKTA YA AFYA UNAOFANYIKA KATIKA VIWANJA VYA KARIMJEE TAREHE 30 JUNI, 2009 –

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii,
Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii,
Makatibu Wakuu,
Makatibu Tawala wa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani,
Wawakilishi kutoka Wadau wetu wa Maendeleo,
Wawakilishi kutoka Taasisi za Kidini na Kujitolea,
Mashirika mbalimbali na Asasi za Kijamii zisizokuwa za Kiserikali,
Wakurugenzi,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

Naomba mpokee shukrani zangu za dhati, kwa kunialika ili niweze kuzindua Mpango Mkakati wa Tatu wa Sekta ya Afya utakaotekelezwa kuanzia mwaka 2009 hadi mwaka 2015. Msisitizo mkubwa wa Mkakati huu ni ushirikiano katika kutekeleza Malengo ya Milenia.

Mkakati huu ni sehemu ya Sera, Sheria, Kanuni na maelekezo ya Serikali ambazo hutoa mwelekeo wa jumla wa maendeleo ya nchi. Hii inajumuisha, Dira ya Taifa hadi mwaka 2025, Mkakati wa Kupunguza Umaskini na Kukuza Uchumi Tanzania (MKUKUTA), mabadiliko katika Utumishi wa Umma na Serikali za Mitaa.

Naamini kwamba, Mkakati huu mpya umezingatia maeneo muhimu ya Sera za Afya zilizopita kama mabadiliko katika Sekta ya Afya.

Wageni waalikwa, mabibi na mabwana:

Mageuzi katika Sekta ya Afya, yalianza mwaka 1994 na yalilenga katika kuboresha usawa katika upatikanaji wa huduma za afya, ubora wa huduma zenyewe na ufanisi katika kutoa huduma zenyewe. Matokeo yake, ni kuimarika kwa afya za watanzania. Mkakati wa Afya ya Msingi, iliridhiwa na Serikali ya Tanzania kwa kuzingatia kuwa, Mkakati huu ni wa gharama nafuu zaidi katika kuboresha afya za watu wanaoishi mjini na vijijini. Lengo ni kuwawezesha wananchi waishi muda mrefu.

Nimeambiwa kwamba, msisitizo mkubwa wa mabadiliko katika Sekta ya Afya, ni kuimarisha huduma za afya katika Wilaya, Mikoa Kanda na Taifa. Pia, mabadiliko haya yanazihusu huduma

za hospitali pamoja na kuimarisha huduma za rufaa kuanzia huduma za Afya ya Msingi. Mageuzi katika Sekta ya Afya, yamesadia kuanzishwa utaratibu wa kushirikisha Sekta ya Afya yote na utaratibu huu umejulikana kama “Mpango Mmoja Shirikishi kati ya Serikali na Wadau” (SWAP). Utaratibu huu umekuwa mbadala wa Miradi Misonge ambayo haikuwa endelevu.

Kwa umuhimu ule ule, nimehakikishiwa kwamba, mageuzi katika Sekta ya Afya ndiyo yaliweka misingi ya kupeleka madaraka Wilayani, kuimarisha Miradi Misonge, Kuanzishwa kwa Bima ya Afya na kuchangia gharama za Huduma za Afya.

Wakati ule ule mageuzi katika Sekta ya Afya, yalipata msukumo kutokana na Mipango ya mageuzi katika Serikali za Mitaa na Utumishi wa Umma. Mageuzi haya yalitokea chini ya Mpango mzima wa Mageuzi wa Serikali ya Tanzania. Hivyo, Mpango wa kupeleka madaraka, uwezo na rasilimali kutoka ngazi za juu kwenda chini, ulioasisiwa mwaka 2001. Mpango huu uliwezesha huduma za afya ngazi ya wilaya, ziwe sehemu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Kwa kuzingatia maendeleo haya, nimeambiwa kuwa kuna haja ya kuwa na mpangilio mzuri wa Mipango yetu, Bajeti, Tathmini na

ufuatiliaji wa pamoja. Hii inatokana na ukweli kwamba, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, haihusiki moja kwa moja na Utekelezaji wa Mipango ya Afya ngazi ya Wilaya. Mpango Kabambe wa Afya katika Halmashauri, ulianzishwa kama nyenzo ya uendeshaji, ambapo Mpango huu unasaidia Serikali na Wadau Wetu wa Maendeleo kupata picha juu ya kazi zinazotekelezwa na Halmashauri zetu. Pia, Mpango wa aina hii umetoa mwanya kwa Wadau mbalimbali kushiriki katika mchakato mzima wa kuandaa, na matokeo yake ni kuwa na huduma bora kwa wananchi.

Wageni waalikwa, mabibi na mabwana:

Wakati Serikali ya awamu ya nne ilipoingia madarakani, tulitoa maelekezo mapya kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Maelekezo hayo yalizingatia mabadiliko ya kijamii na kiuchumi, magonjwa mapya na yale yanayoibuka upya baada ya kuwa yamepungua, na vilevile mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia. Maelekezo yaliiwezesha Serikali, kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kupitia upya Sera ya Afya ya mwaka 1990, ambapo Sera Mpya ya Afya ya mwaka 2007 ilikamilishwa na kuidhinishwa na Mamlaka zinazohusika. Dira ya Sera iliyopitishwa ni kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi ambayo uchangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya nchi. Pia, makusudio ya Sera mpya ni kutoa huduma muhimu za afya zenye

uwiano wa kujiografia, viwango vya ubora unaokubalika,kwa gharama nafuu na huduma zilizo endelevu.

Huduma za afya, zinalenga watu walio katika hatari zaidi ili waweze kupata huduma zilizo bora na karibu wanapoishi. Hii, itasaidia kuboresha ubora wa maisha yao, na hivyo kupunguza magonjwa ya kuambukiza na kuongeza umri wa kuishi wa Mtanzania.

Serikali ya Tanzania, ilihakikisha kwamba, Sera ya Afya iliyopitiwa ya mwaka 2007, ilitumika wakati wa kuandaa Mpango mpya wa Afya ya Msingi ambao umejulikana kama MMAM 2007 – 2017 (Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi). Lengo la MMAM, ni kuendeleza utoaji wa hudumza za afya ya msingi kwa watu wote ifikapo mwaka 2012, na katika miaka mitano iliyobaki, mpango utatumika katika kuimarisha mafanikio yatakayokuwa yamefikiwa. Hapa msisitizo mkubwa ni kuimarisha mifumo ya afya iliyopo, kwa kuhakikisha kila kijiji na kila kata inakuwa na kituo cha kutolea tiba kilicho karibu na wananchi. Kuimarisha mfumo wa rufaa, kuendeleza nguvu kazi na kuipeleka huko inapohitajika, kuongeza bajeti ya afya kupanua upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika ngazi zote.

Wageni waalikwa, mabibi na mabwana:

Nimefahamishwa kwamba, Mpango Mkakati wa Tatu wa Sekta ya Afya ambao nitauzindua leo, utachukua pahala pa Mpango Mkakati wa Pili wa Sekta ya Afya, ambao ulitoa mwelekeo wa maendeleo ya Sekta ya Afya kuanzia mwaka 2003 hadi Juni, 2009. Katika miaka sita iliyopita, msisitizo ulikuwa kuimarisha huduma za afya ngazi ya wilaya, kuanzisha mageuzi ya hospitali, kuimarisha Makao Makuu ya Wizara, Mifumo ya kusaidia huduma za afya, maendeleo ya nguvu kazi kwa ajili ya huduma za afya, na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Sekta, kupanua ushirikiano kati Serikali na Sekta Binafsi, kuimarisha uratibu wa Sekta, kukinga na kuthibiti Malaria, Kifua Kikuu na Ukoma, huduma na Mama na Mtoto na kupanua Mpango wa kudhibiti UKIMWI.

Pia, nimefahamishwa kwamba, tathmini ya Sekta ya Afya iliyofanywa na watathmini kutoka nje ya nchi ya mwaka 2007 ikiratibiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi ilitoa matokeo yaliyo mazuri. Serikali ilifarijika kuona kwamba, maeneo mengi ambayo tumepiga hatua, yalidhibitishwa na timu ya wataalam kutoka nje ya nchi. Mfano mzuri ni Vifo vya watoto wachanga chini ya miaka mitano vilipungua kutoka vifo 147 mwaka 1999 hadi vifo 112 mwaka 2004 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai. Vifo katika umri huu, viliendelea kupungua zaidi hadi kufikia vifo 91 katika mwaka 2007/2008. Pia, vifo vya watoto chini ya umri wa mwaka

mmoja navyo vilipungua kutoka vifo 99 mwaka 1999 hadi 68 mwaka 2004/05 kati ya watoto 1000 wanaozaliwa wakiwa hai. Katika miaka 3 iliyofuata vifo vilipungua zaidi hadi kufikia vifo 58 kwa mwaka 2007 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa wakiwa hai. Aidha, vifo vya watoto wenye umri wa siku 28, navyo vilipungua kutoka vifo 38 mwaka 2004/05 hadi vifo 29 mwaka 2007 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai. Huu ni udhibitisho tosha kwamba, bado tuna nafasi ya kufanya maboresho katika mifumo yetu ya afya ili kupata maendeleo zaidi ya kufikia malengo ya Milenia, hususani yanayohusu vifo vya akina mama vinavyosababishwa na uzazi. Pamoja na wananchi kupata huduma za afya, pia ubora wa huduma zenyewe utahitajika, ili kupata mafanikio zaidi. Hii itahusu maendeleo ya watumishi katika Sekta ya Afya kwa kuongeza idadi yao na wenye mchanganyiko wa taaluma mbalimbali. Mpango huu pia, hapana budi kuendelezwa katika mkakati huu. Mabadiliko katika uendeshaji wa mifumo ya afya yalikuwa ni muhimu ili kuendeleza mageuzi ya hospitali yanayoendelea hadi sasa, yakiwa na lengo la kuendeleza ushirikiano kati ya Serikali na Sekta za Watu Binafsi. Mapendekezo yaliyotokana na ripoti ya tathmini, yalikuwa mapendekezo mazuri, kwani yalionyesha kuwa, tuna mifumo ya afya iliyo imara na inayoweza kuboresha huduma za afya hapa nchini. Nawapongeza wale wote walioshiriki katika kufanya tathmini hiyo.

Wageni waalikwa, mabibi na mabwana:

Mimi mwenyewe na Serikali kwa ujumla, tunakiri kwamba, Sekta ya Afya ni kubwa na ina maeneo mengi ambayo yanahitaji kufanya kazi kwa pamoja. Hii inadhihirishwa na mtaji mkubwa unaowekwa na Serikali. Kwa kuwafahamisha zaidi, bajeti ya Serikali imefikia asilimia 11.6 na kwa kipaumbele. Sekta ya Afya, imeendelea kuwa ya tatu kwa umuhimu. Serikali ya Tanzania itaendelea kuongeza bajeti katika sekta ya afya na itahakikisha inabaki nafasi si chini ya tatu kwa umuhimu.

Kwahiyo, ninachokiona kwa leo ni ukweli kwamba maendeleo ya Mpango Mkakati wa Tatu wa Sekta ya Afya 2009 – 2015 kwa kiwango kikubwa umezingatia matarajio ya wananchi, ukubwa wa kazi iliyo mbele yetu ya kupambana na changamoto zilizomo, ukubwa wa Sekta yenyewe na mchango wa wadau mbalimbali waliohusishwa. Hii inahakikisha kwamba patakuwepo na ongezeko la utoaji wa huduma za afya zitolewazo na zilizo bora. Matokeo yake watanzania kuwa na afya bora.

Naamini kwamba, maandalizi ya Mpango Mkakati wa tatu wa Sekta ya Afya umepata bahati ya kuchangiwa na wataalamu mbalimbali kutoka sekta zingine, wawakilishi wa jamii, wadau wetu wa Maendeleo, Asasi za kijamii na mashirika ya dini ambao

wengi wao wapo hapa. Nawashukuru kwa ushirikiano ambao umelenga kuboresha sekta ya Afya.

Mpango Mkakati III wa Sekta ya Afya, unalenga katika kuleta mabadiliko makubwa katika nchi yetu katika kutoa huduma za Afya ya Msingi, kwa kuhakikisha kuwa zinatolewa kwa usawa. Huduma hizo, zitahusisha kuhamasisha wananchi, kutoa kinga ya maradhi, pamoja na huduma za matibabu.

Kuwapo kwangu leo, kunawahakikishia kwamba kuna utashi wa kisiasa, katika kutekeleza Mpango Mkakati wa III wa Sekta ya Afya na Serikali yetu. Pia, hii inadhihirisha kwamba Mpango huu upo chini ya umiliki wa nchi yetu. Aidha, kuwepo kwa Washirika wa Maendeleo na Wadau mbalimbali, ni uthibitisho kwamba kuna ushirikiano imara kupitia Mpango mmoja shirikishi kati ya Serikali na Wadau mbalimbali. Nataka kuwahakikishia kwamba, kutokana na Mpango huu patakuwepo na matokeo yanayoonekana ambao wote tunawajibika nayo.

Kwa hiyo, naitaka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhakikisha kwamba, Mkakati wa tathmini na ufuatiliaji katika ngazi zote ni imara ili kuwezesha kujua matokeo ya mkakati mzima. Hadi sasa, naridhika na baadhi ya matokeo yanayoonyesha kwamba tumepiga hatua katika Sekta ya Afya, hii

haitoshi na ndio maana tunatoa nafasi kwa mkakati huu mpya, ili uwe chachu ya maendeleo tukitarajia kupata matokeo yaliyo bora katika Sekta ya Afya.

Nawaomba washirika wetu maendeleo waendelee kusaida Serikali yetu kwa kuongeza fedha za kutekeleza Mpango huu. Mpango hata uwe mzuri kiasi gani bila fedha za utekelezaji siyo Mpango. ***A plan is not a plan unless is funded.***

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana

Ninatoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa wahisani wetu na wadau wetu kwa kushiriki kuchangia fedha ya afya kwa njia mbalimbali. Kuchangia kupitia "Health Basket Fund" ni utekelezaji mzuri wa makubaliano ndani ya Mkakati wa Pamoja na kusaidia Serikali ya Tanzania (JAST). Mfuko huu umeongezeka kukua kuanzia dola za Kimarekani 25 millioni 2003 hadi kufikia dola za Kimarekani 61 millioni 2009. Hili ni ongezeko kubwa sana kwa kipindi hicho. Ninawashukuru tena Wahisani wetu.

Nafahamu, wahisani hawa pia wanatoa mchango wao moja kwa moja kwenye bajeti ya serikali *(General Budget Support – GBS)* ambayo ni njia muhimu ya kutoa mchango kwa serikali.

Mpango mkakati huu una pengo la asilimia ishirini (20%) ya bajeti yake ya utekelezaji kwa miaka yote sita.

Nachukua fursa hii kuwaomba Wahisani wetu kuongeza michango yao kuziba pengo hili. Pamoja na kuporomoka kwa uchumi wa dunia. Kuchangia afya ni kigezo cha kupima ubinadamu wetu.

Kwa kila Mtanzania, bajeti imeongezeka kutoka dola za kimarekani 5 hadi 14 kwa kipindi cha miaka tisa iliyopita, hata hivyo fedha zaidi zinahitajika kuimarisha sekta hii. Nawashukuru tena kwa mchango wenu. Baada ya kuzindua Mpango Mkakati huu wa tatu, kazi kubwa itabakia kwa watekelezaji na wasimamizi kuhakikisha mambo muhimu yameingizwa kwenye mipango kazi, inatekelezwa na kusimamiwa vema.

Kazi kubwa itafanyika ngazi ya wilaya, mkoa Kanda na Taifa. Sera ya Serikali ni kuimarisha wilaya kwa mfumo wa D by D hili lizingatiwe. Wizara zitaendelea kutoa utaalamu, usimamizi na ufuatiliaji kulingana na vigezo vilivyowekwa. Ngazi ya mkoa timu zao za usimamizi zitaendelea kusimamia hospitali za mikoa na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa halmashauri husika. Hili ni kuhakikisha Sera na Mikakati inatekelezwa kama tulivyokubaliana, pia kuhakiki ubora na upatikanaji huduma vijijini.

Mkakati huu ni wa kuzingatia na watekelezaji wote, ndani ya Serikali na Wadau ili kuhakikisha ubora wa huduma za Afya.

Natoa tena shukrani zangu za dhati kwa washirika wetu wa maendeleo, wadau na wale wote walioandaa Mpango huu, na mliofika kushuhudia uzinduzi wake.

Sasa natamka rasmi kuwa **MPANGO MKAKATI WA TATU WA SEKTA YA AFYA 2009 – 2015** umezinduliwa rasmi.

AHSANTENI !